# RIPOTI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha106 (e) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012. Majukumu ya Kamati yameelezewa katika kanuni ya 112 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi ambapo miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kama yafuatayo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswaada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika .

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ina jukumu la kufuatilia utekelezaji katika Wizara tatu nazo ni kama ifuatavyo:-

1) Wizara ya Afya

2) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

3) Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Kama kawaida kwa mwaka huu wa Fedha 2014/2015 Kamati ilifanya kazi zake Unguja kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 10/07/2014 mpaka tarehe 23/07/2014 na kwa upande wa Pemba ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 08/12/2014 mpaka tarehe 19/12/2014. Vile vile Kamati ilimazia mzunguko wake wa mwisho wa kazi kwa upande wa Unguja kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 02/02/2015 mpaka tarehe 13/02/2015.

## WAJUMBE WA KAMATI

Kamati ina wajumbe saba na makatibu wawili kama wafuatavyo-:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hassan Hamad Omar | Makamo Mwenyeki |
| 3. | Mhe. Ali Salum Haji | Mjumbe. |
| 4. | Mhe. Abdi Mosi Kombo | Mjumbe. |
| 5. | Mhe. Farida Amour Mohamed | Mjumbe. |
| 6. | Mhe. Mohamed Mbwana Hamad | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mwanaid Kassim Mussa | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Abubakar Mahmoud Idd | Katibu |
| 9. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |

## SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA AFYA

Wizara ya Afya imeundwa na Idara zifuatazo:-

1. Idara ya Kinga na Elimu ya Afya.
2. Idara ya Tiba.
3. Idara ya Hospitali ya Mnazi mmoja.
4. Idara ya Bohari kuu ya Dawa.
5. Idara ya Sera, Mipango na Utafiti.
6. Idara ya Utumishi na Uendeshaji.

Wizara pia ina Taasisi Maalum ambazo miongoni mwao ni Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Baraza la Wauguzi na Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala.

Katika Wizara hii, Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilikutana na watendaji wa Wizara ya Afya Unguja na watendaji wa Ofisi kuu Pemba na kujadili utekelezaji wa shughuli za Wizara. Aidha Kamati ilitembelea maeneo mbali mbali yaliyopo Unguja na Pemba kwa ajili ya kujiridhisha na utekelezaji wa shughuli za Wizara.

## IDARA YA TIBA

Kamati ilielezwa kuwa, Idara hii ya tiba inajumuisha hospitali tatu za Wilaya ambazo ni Hospitali ya Chake Chake, Hospitali ya Abdalla Mzee na Hospitali ya Wete, Pia inahusika na hospitali nne za vijiji ambazo ni Hospitali ya Makunduchi, Kivunge, Micheweni na Vitongoji. Aidha Idara inajumuisha mpango wa damu salama, usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi, mradi wa chuo cha madaktari Zanzibar na mradi wa kuzipandisha hadhi Hospitali za vijiji na Hospitali za Wilaya.

Kamati ilifanikiwa kukagua baadhi ya maeneo yaliyopo chini ya Idara hii na kubaini changamoto mbali mbali ambazo zinakwamisha jitihada za Wizara katika kuhakikisha kuwa huduma bora na salama zinapatikana kwa wananchi.

### CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI HOSPITALI YA MAKUNDUCHI

### (MAKUNDUCHI COTTAGE HOSPITAL)

1. **Ufinyu wa Bajeti:** hii ni changamoto kubwa ambayo Kamati imekuwa ikikabiliana nayo kwa Wizara zote tatu ambazo inazisimamia. Katika Hospitali ya Makunduchi kiwango cha fedha wanachopatiwa hakilingani na kile kiwango cha fedha walichokiomba kwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Kwa mfano ufinyu wa fedha katika Hospitali imepelekea gari la kubebea wagonjwa kukosa mafuta ipasavyo na kukwamisha utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

2. **Uhaba wa nyumba za madaktari**: Kamati pia imebaini kuwa uhaba wa nyumba za Madaktari katika Hospitali ya Makunduchi unapelekea madaktari kujibana katika nyumba chache zilizopo hali ambayo inahatarisha usalama wa afya zao pamoja na mali zao.

3. **Uhaba wa madawa na vitendea kazi:** Kamati pia imebaini kuwa Hospitali ina uhaba wa madawa, vifaa vya maabara na vifaa vya kusafishia kama vile sabuni na jiki hali inayozorotesha utekelezaji wa shughuli za Hospitali.

4. **Kukosekana kwa Walinzi na uzio:** Kamati imesikitishwa sana kuona kwamba Hospitali imekosa ulinzi na usalama kwani imebaini kuwa kuna vitendo vya wizi vinavyotokea ambavyo hupelekea kupotea kwa baadhi ya vifaa. Aidha kukosekana kwa uzio kumepelekea wanyama kama mbuzi na mbwa kuingia ovyo katika maeeo ya Hospitali.

5. **Ufinyu wa Nafasi ya Maabara:** tatizo hili linachangia kuwepo kwa usumbufu wakati wa kutoa huduma kutokana na kuwa sehemu ya maabara ni finyu na inaathiriwa sana na vumbi hali inayopelekea kuharibika kwa baadhi ya vifaa na watendaji kupata wakati mgumu wakati wa kutoa huduma.

6. **Uchache wa Magari ya kubebea wagonjwa:** Kamati ilipofanya ziara zake ilijionea kuwa Hospitali ina gari moja tu ya kubebea wagonjwa ambayo haikidhi haja kwani idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa wameongezeka hususani wale ambao wanahitaji kufanyiwa utaratibu wa rufaa kwenda Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja. Kwa mfano katika kipindi cha siku za nyuma hospitali ilikuwa inatoa rufaa ya wagonjwa nane tu kwa mwezi lakini kutokana na ongezeko la wagonjwa, kwasasa idadi hiyo imefikia wagonjwa ishirini mpaka thalathini kwa mwezi.

7. **Uhaba wa wafanyakazi**: Kamati imeshtushwa na jambo hilo kwani Hospitali ina jumla ya wafanyakazi sabini na moja tu wakati inahudumia wagonjwa wengi. Kwa msingi huo kumekuwa hakuna uwiano kwa watendaji waliyopo na wagojwa wanaohudhuria kwa ajili ya kupatiwa huduma Hospitalini. Kamati imebaini kuwa, upungufu huo wa wafanyakazi umejitokeza hasa katika kada ya ukunga ambapo waliopo ni wanne tu kinyume na mahitaji halisi ya Hospitali hiyo.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Wizara kuongeza idadi ya nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Makunduchi ili wafanyakazi wapate makazi ya kutosha na kuweza kukaa katika sehemu ambazo zitalinda usalama wa afya zao na mali zao.
2. Kamati inaitaka Wizara kuongeza gari ya kubebea wagonjwa katika Hospitali ya Makunduchi kulingana na mahitaji halisi ya hospitali kwani gari moja liliopo sasa halikidhi haja.
3. Kamati inaitaka Wizara kuizungushia uzio Hospitali ya Makunduchi ili kuimarisha ulinzi katika hospitali hiyo na kuepusha uingiaji ovyo wa wanyama katika maeneo ya hospitali.
4. Kamati inaishauri Wizara kuongeza idadi ya wafanyakazi wakiwemo wakunga na walinzi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa tiba pamoja na usalama wa majengo na mali katika Hospitali ya Makunduchi.

**CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KITENGO CHA AFYA YA MAZINGIRA**

1. **Ufinyu wa Bajeti**: Kamati imebaini kuwa kitengo kinakabiliwa na ufinyu wa bajeti hali inayokwamisha utekelezaji wa shughuli zao kwa ufanisi.
2. **Ufinyu wa nafasi**: Kamati imebaini kuwa kitengo kinakabiliwa na tatizo la nafasi hali inayopelekea watendaji wa kitengo kukaa katika vitengo vyengine.
3. **Tatizo la usafiri**: Kamati imebaini kuwa kitengo kinakabiliwa na tatizo la usafiri hali inayokwamisha kazi za ufuatiliaji na utoaji wa elimu katika sehemu za vijijini.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Wizara kukipatia kitengo usafiri ili kiweze kutekeleza kazi za ufuatiliaji na utoaji wa elimu hasa katika maeneo mbali mbali ikiwemo ya vijijini.
2. Kamati inakishauri kitengo cha Afya ya mazingira kufanya mashirikiano na taasisi nyengine zinazojishughulisha na masuala ya mazingira kama vile Wizara ya Elimu, halmashauri za miji pamoja na Manispaa ili kwa pamoja waweze kutoa elimu ya kutunza mazingira kwa ajili ya kuboresha mazingira na Afya za binaadamu.

**IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**

Katika kuangalia maendeleo na matatizo ya huduma ya Afya katika Hospitali ya Mnazi mmoja, Kamati ilibahatika kukagua Wodi ya Wagonjwa wa Sukari, Wodi ya wagonjwa wa Mifupa, Wodi ya Wazazi, Wodi ya Wagonjwa Mahtuti (ICU) ya Zamani na Wodi ya

Wagonjwa Mahtuti (ICU) Mpya. Katika maeneo hayo Kamati imeziona juhudi zinazochukuliwa na Watendaji wa Idara hizo licha ya kukabiliwa na changamoto, Idara inaendelea kujitahidi na kuhakikisha kuwa inatoa huduma kwa wagonjwa wanaojitokeza.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WODI YA WAGONJWA WA SUKARI**

1. Hali ya wodi hairidhishi kwa Afya ya wauguzi pamoja na wagonjwa kwa ujumla kwani mazingira hayapo salama ya usafi kutokana na uhaba wa vitendea kazi (gloves,jiki, mashuka) hali ambayo inaweza kusababisha maambukizi ya maradhi mengine.
2. Kamati ilipotembelea wodi ya wagonjwa wa sukari (sehemu ya wanawake na wanaume) ilibaini uchakavu wa wodi, uhaba wa vitendea kazi na baadhi ya mafeni yaliyopo katika wodi hizo kutofanya kazi.
3. Kukosekana kwa dawa za wagonjwa wa sukari. Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya siku hospitali inakuwa haina dawa za wagonjwa wa sukari hali inayopelekea wagonjwa kulazimika kununua dawa wenyewe.
4. Kamati pia imekutana na changamoto ya vifaa vya kufungia vidonda kwa wagonjwa (dressing equipment) kwani kazi kubwa ya wodi hizo ni kufunga na kusafisha vidonda.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kuzifanyia matengenezo wodi hizo na kuzipatia vifaa vya kutosha ili watendaji wafanye kazi zao kwa usalama wa Afya zao na wagonjwa.
2. Wizara iwe na utaratibu mzuri wa kujenga hoja madhubuti Serikalini ili bajeti ya dawa iongezwe na iweze kusaidia wagonjwa hasa wagonjwa ambao wana kipato cha chini.

**CHANGAMOTO INAZOZIKABILI WODI YA WAGONJWA WA MIFUPA**

1. Upatikanaji mdogo wa vifaa vya matibabu ya wagonjwa wa mifupa kutoka Serikalini.
2. Uhaba wa Wauguzi na madaktari wa mifupa ni changamoto kubwa inayoikabili wodi hii, kwani muuguzi mmoja hutoa huduma katika wodi nzima na hivyo hujikuta anafanya kazi nyingi ambazo zipo nje ya uwezo wake, hatimae huduma haziwafiki walengwa katika kiwango kinachostahiki.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Hospitali ya Mnazi mmoja vifaa vya matibabu ya mifupa kutokana na kuwa, vifaa hivyo ni ghali na mwananchi wa kawaida hawezi kuvimudu. Aidha Kamati inaitaka Wizara kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika na usalama barabarani kutoa elimu kwa jamii ili kupunguza idadi ya ajali barabarani zinazopelekea ongezeko la idadi ya wagonjwa wa mifupa nchini.
2. Kutokana na tatizo la uhaba wa wataalamu wa mifupa, Kamati inaiagiza Serikali kutafuta mtaalamu wa mifupa haraka iwezekanavyo na kuwashajihisha watendaji kujiendeleza katika fani ya mifupa, kwani matatizo ya mifupa kwa sasa yamekua yakijitokeza mara kwa mara katika nchi yetu.

## WODI YA WAGONJWA MAHTUTI KONGWE (ICU)

1. Kamati ilipotembelea wodi ya wagonjwa mahtuti kongwe ilibaini upungufu wa watendaji ambapo kwasasa kuna muuguzi mmoja na mahitaji ya wodi ya ICU hiyo ni wauguzi watano ili kila mgonjwa aweze kupatiwa huduma nzuri na uangalizi wa kutosha.

## MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kuongeza watendaji katika wodi ya wagonjwa mahtuti kongwe kwasababu muuguzi mmoja hatoshi katika kuwahudumia wagonjwa watano kwa wakati mmoja na inakuwa ni vigumu kwa muuguzi kutoa huduma iliyo bora kwa wagonjwa wote kwani taratibu za utoaji huduma bora ya afya huzingatia zaidi idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI HOSPITALI YA KIDONGO CHEKUNDU

1. Kamati ilipotembelea jiko jipya katika hospitali hii ilibaini kukosekana kwa kifaa cha kuzimia moto (fire extinguisher). Kifaa ambacho ni muhimu kutokana na kuwa jiko limejengwa kisasa na linatumia majiko ya gesi kwa kupikia.
2. Hospitali ina upungufu wa madaktari. Kwasasa kuna daktari mmoja tu wa kizalendo aliyebobea katika magonjwa ya akili. Aidha kuna upungufu wa wauguzi hali inayopelekea baadhi ya muda wodi kuhudumiwa na maodali tu hali ambayo haikubaliki katika maadili ya kazi za uuguzi.
3. Kitengo kipya cha methodonic (kitengo cha matibabu ya watumiaji wa madawa ya kulevya) kutokuwa na vitendea kazi (vifaa vya maabara, viti, meza). Hii ni changamoto kwa kitengo hicho kipya kwani hali hii itasababisha watoa huduma katika kitengo hicho kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi na hatimae kutofikiwa malengo yaliyokusudiwa.

## MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiagiza Wizara kuipatia Hospitali ya Kidongo chekundu kifaa cha kuzimia moto (fire extinguisher) na kuwapatia watendaji wake taaluma ya kujikinga na ajali ya moto hasa wale wanaoshughulika na kazi za jikoni ili iwasaidie katika kupambana na janga la moto pindi litakapotokezea.
2. Kamati inaishauri Wizara kuwashajihisha watendaji wake kusomea fani ya magonjwa ya akili kutokana na kuwa, fani hii ina upungufu mkubwa na magonjwa ya akili yamekuwa yanaongezeka nchini.
3. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha kitengo cha methodonic kwa ajili ya kuwapatia matibabu watu waliothirika na madawa ya kulevya hasa wale wanaotumia madawa hayo kwa kujidunga. Kamati inaitaka Wizara kukiimarisha kitengo hicho kwa kukipatia vifaa vilivyokuwa na upungufu ili malengo yaliyokusudiwa ya kuanzisha kitengo hicho yafikiwe na kuwasaidia vijana ambao ndio nguvu kazi katika kupambana na janga hilo.

## BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI

Kamati ilitembelea ujenzi wa Ofisi Mpya ya Bodi ya Chakula, Dawa na vipodozi na ilifurahishwa na hatua iliyofikiwa. Aidha Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli zao na kubaini changamoto zifuatazo:-

1. Sheria Namba 2 ya mwaka 2006 ya chakula, Dawa na Vipodozi kupitwa na wakati. Kamati ilibaini kuwa, Bodi tayari imeshachukua jitihada ya kuipeleka sheria hiyo kwa makatibu wakuu kwa ajili ya kuipitia tokea mwezi wa Oktoba 2013 lakini Kamati imebaini kuwa sheria hiyo bado haijafanyiwa kazi.
2. Bodi kutopatiwa ruzuku kutoka Serikalini na hivyo fedha wanayotumia katika kazi zao za kila siku zinatokana na makusanyo yanayofanywa na Bodi.
3. Kukosekana kwa maji katika Ofisi Mpya ya Bodi na hivyo kulazimika kununua maji kwa matumizi ya Ofisi.
4. Kamati imebaini kuwa, licha ya kuwa Bodi wameanza kutumia Ofisi yao mpya lakini sehemu ya nje ya jengo inahitaji kufanyiwa ukarabati. Aidha jengo linahitaji kupatiwa samani kama vile viti, meza na makabati.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaiagiza Wizara kuharakisha marekebisho ya Sheria namba 2 ya mwaka 2006 ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambayo imeshapelekwa kwa makatibu wakuu kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho tokea mwaka 2013. Aidha Kamati inaitaka Wizara kuharakisha marekebisho hayo kwasababu nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizotiliana mikataba ya kuwa na sheria zinazofanana katika sekta ya afya ikiwemo Tanzania, Kenya, Unganda na Rwanda wameshabadilisha sheria zao za Bodi isipokuwa Zanzibar tu.
2. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Bodi ruzuku ili iweze kutekeleza kazi walizojipangia kwa ufanisi kwani fedha zinazokusanywa na Bodi pekee hazitoshelezi katika utekelezaji wa majukumu yao.
3. Kamati inaitaka Wizara kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika Bodi kwani maji ni muhimu sana katika shughuli zao za kila siku hasa za maabara. Mbali na changamoto ya maji, Kamati inaitaka Wizara kuwapatia watendaji wa Bodi viti, meza na makabati ili kuondosha mapungufu ya vifaa hivyo.

**OFISI KUU PEMBA**

Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Uongozi wa Ofisi kuu Pemba na kupokea taarifa ya utekelezaji, kutembelea kituo cha Afya cha Kojani, kituo cha Afya cha Ukutini na Maabara ya Mkemia Mkuu. Kamati wakati wa kupokea taarifa pamoja na kufanya ukaguzi wa maeneo ya wizara ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Kamati imebaini uingizwaji wa fedha usio wa kuridhisha unazorotesha utekeelezaji wa majukumu ya Wizara.
2. Kamati imebaini kuwa kukosena kwa jengo la Ofisi kwa ajili ya shughuli za Wizara ni tatizo kubwa linaloikabili Ofiku Kuu Pemba kwani ofisi zao zipo katika jengo la hospitali ya Wete

ambazo ni finyu na watendaji wanakosa ufanisi wa kazi zao kutokana na kuwa hakuna utulivu wa kutosha.

3. Kamati pia imebaini tatizo la upatikanaji wa dawa katika Hospitali na vituo vya afya pamoja na uchakavu wa gari la kusambazia madawa.
4. Kamati imetambua kuwa, kuna upungufu wa vitendea kazi (reagents,autoclaves nk) na wataalamu kama matabibu wa meno,wafamasia,wataalamu wa mionzi na wataalamu wa viungo katika vituo vya afya na hospitali.
5. Kamati imebaini kukosekana kwa tanuri la kuchomea taka za hospitali na kupelekea taka kuchomwa katika mashimo.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara ya Afya - Pemba Jengo la Hoteli ya Wete kwa ajili ya matumizi ya Ofisi kwani kwa kipindi kirefu jengo hilo limekuwa halitumiki. Aidha Kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara Jengo la Hoteli ya Mkoani ili litumike kwa ajili ya makaazi kwa watendaji wa Wizara ya Afya Pemba.
2. Kamati inaitaka Wizara kuirudisha kozi ya ukunga iliyokuwa inatolewa katika chuo cha Afya Mbweni ambapo kwasasa imefutwa ili kupunguza tatizo la kukosekana kwa wakunga katika vituo vya Afya.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KITUO CHA AFYA CHA KOJANI**

1. Kamati ilipotembelea Kituo cha Afya cha Kojani, kimebaini uhaba wa wataalamu kama vile (dentist, wakunga, mtaalamu wa maabara na mtaalamu wa madawa) kumepelekea kituo kukosa kutoa huduma hizo ipasavyo na baadhi ya huduma kutotolewa kabisa.
2. Kukosekana kwa usafiri wa uhakika kwa ajili ya kubebea wagonjwa ni tatizo kubwa ambalo linakikabili kituo hasa kunapotokea mgonjwa wa dharura ambaye anahitaji kupatiwa matibabu zaidi katika Hospitali za Rufaa.
3. Kamati imesikitishwa sana kuona kituo kinakosa ulinzi kwani wafanyakazi wengi waliopo katika kituo hicho ni wanawake na hupata hofu kubwa juu ya usalama wao na vifaa vilivyopo katika kituo hasa wakati wa usiku.
4. Kamati imeona hali halisi ya nyumba za wafanyakazi zilizopo Kojani ambazo ni mbovu na chakavu na kupelekea wafanyakazi kushindwa kuishi katika nyumba hizo.

**CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KITUO CHA AFYA CHA UKUTINI**

1. Kamati ilipotemnbelea Kituo cha Afya cha Ukutini kilibaini kukosekana kwa wafanyakazi wa kutosha katika kada ya wafamasia, wataalamu wa maabara na wataalamu wa meno.
2. Kamati imebaini kuwa kituo kinakabiliwa na ukosefu wa vifaa kama vile vitanda, mashuka, meza, viti na mashine ya kupimia damu hali inayopelekea kituo kukosa ufanisi katika kuwapatia huduma wagonjwa.

3. Kamati imebaini kuwa, kituo kina tatizo la kukosa usafiri wa uhakika kwa ajili ya kubebea wagonjwa hali inayohatarisha usalama wa wagonjwa hasa wa dharura (mahtuti).

4. Kamati imebaini kuwa Kituo kinakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji hali inayopelekea kituo kushindwa kutoa huduma ya kujifungu (kuzalisha). Aidha kituo kinashindwa kutoa huduma za kujifungua kutokana na uhaba wa vifaa.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati ilipokuwa inatembelea vituo vya afya, imebaini kuwa vituo vinakosa wafanyakazi wa kutosha na ni tatizo kubwa ambalo linavikabili vituo vingi vya afya na kupelekea utoaji wa huduma usio wa kuridhisha, hivyo Kamati inaishauri Wizara kuvikagua vituo vyake mbali mbali na kubaini mapungufu yaliyopo na hatimae kuchukua hatua za kurekebisha mapungufu hayo.

2. Kamati inaitaka Wizara kukiwezesha Kituo cha Afya cha Ukutini kwa kukipatia vifaa na kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji ili kituo kiweze kutoa huduma mbali mbali ikiwemo za kujifungua.

3. Kamati imebaini kuwa, baadhi ya vituo vya afya havina ulinzi na inaitaka Wizara kuendelea kuishajihisha jamii kufanya juhudi ya kuvilinda vituo vyake ili kupinga vitendo vya wizi vinavyotokea katika vituo hivyo.

4. Kamati inaitaka Wizara kuchukua hatua za haraka za kurekebisha nyumba za madaktari zilizopo Kojani kwani nyumba hizo haziridhishi na wafanyakazi wanashindwa kuzitumia.

5. Kamati imebaini kuwa vituo vya afya vinakosa usafiri wa uhakika kwa ajili ya kubebea wagonjwa hali inayohatarisha maisha ya wagonjwa. Hivyo kamati inaitaka Wizara kuvipatia vituo usafiri wa uhakika hasa vituo vilivyopo katika maeneo ya visiwa kwani watendaji wa vituo hivyo wanakuwa katika wakati ngumu pindi wanapokuwa na mgonjwa wa dharura anaehitaji kupatiwa rufaa na ambapo kunakuwa hakuna usafiri wa uhakika wa majini na nchi kavu.

**CHANGAMOTO INAZOZIKABILI OFISI YA MKEMIA MKUU PEMBA**

1. Kamati ilipotembelea Ofisi ya mkemia Mkuu Pemba imebaini uhaba wa Wachunguzi wenye ujuzi wa juu (speciality) kwenye fani ya uchunguzi wa vyakula, sumu pamoja na kesi za jinai.

2. Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Mkemia ni finyu hali iliyopelekea kukodi jengo jengine kwa ajili ya matumizi ya ofisi ambapo kodi yake inagharimu milioni 12 kwa mwaka.

3. Kamati imebaini kuwa ofisi ya Mkemia Mkuu haina maabara ya kudumu kwa ajili ya kufanyia shughuli zake ambapo kwasasa maabara hiyo iko kwenye maeneo ya Hospitali ya Chake chake na Ofisi za Maabara ya Mkemia Mkuu ziko kwenye jengo la kukodi liliopo Miembeni Chake chake Pemba.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI.**

3. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha ujenzi wa Ofisi ya Mkemia Mkuu Pemba ili kupunguza gharama za kulipa kodi ya Ofisi ya Maabara ya Mkemia ambayo kwa mwaka ni milioni kumi na mbili.

4. Kamati inaitaka Wizara kuwasomesha wataalamu waliopo katika Maabara ya Mkemia Mkuu Pemba ili waweze kubobea katika fani mbali mbali za uchunguzi ikiwemo uchunguzi wa vyakula, sumu na uchunguzi wa kesi za jinai ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kupunguza gharama za kusafirisha sampuli Dar es salam kwa ajili ya uchunguzi.

**WIZARA YA UWEZESHAJI, USTAWI WA JAMII, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO**

Kamati ilifanya ziara katika Wizara ya Uwezeshaji, ustawi wa Jamii, Vijana, wanawake na Watoto na kupokea taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai/Septemba 2014/2015 kwa upande wa Pemba na kwa upande wa Unguja ilipokea taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Oktoba/Disemba 2014/2015. Kamati katika shughuli zake pamoja na kukagua maeneo mbali mbali, ilikutana na Kitengo cha Jinsia kwa lengo la kupata maelezo ya Kitengo ikiwemo mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na udhalilishaji na namna zinavyoratibiwa katika ngazi zote.

Pia Kamati ilikutana na wahusika wanaoshughulikia uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa watoto na kumalizia ziara yake kwa kutembelea Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi kichumi, Idara ya Wanawake na Watoto, Idara ya Maendeleo ya Vijana na Idara ya ustawi wa Jamii.

Kamati ilipokutana na wahusika wanaoshughulikia uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa watoto (Wizara, Polisi na Mkurugenzi wa Mashtaka) iliweza kubaini changamoto zifuatavyo katika uendeshaji wa kesi hizo:-

1. Kamati imebaini kuwa, kukosekana kwa kifaa cha DNA kunapelekea kutopatikana kwa ushahidi wa kitaalamu kwa kesi za udhalilishaji hasa kwa kesi za watoto ambao wana magonjwa ya akili na ambao hawana uwezo wa kujieleza mpaka kupatikane kwa vipimo vya DNA kwa ajili ya uchunguzi na kupatikana na majibu ya kipimo hicho yanasaidia katika kutoa ushahidi.

2. Kamati imebaini kuwa upungufu wa wafanyakazi katika Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto na washauri nasaha ni tatizo ambalo linahitaji kufanyiwa ufumbuzi wa haraka kwani kitengo hicho ni muhimu katika kuwapatia huduma za nasaha watoto hasa katika kipindi hichi ambacho kumekuwa na ongezeko kubwa la kesi za udhalilishaji wa watoto

3. Kamati imetambua kuwa, hakuna sehemu maalum kwa ajili ya kuwaweka wahanga wa vitendo vya udhalilishaji wakati wakiendelea kupatiwa huduma mbali mbali zikiwemo za ushauri nasaha.

4. Kamati iligundua kuwa, uhamisho wa polisi katika vituo vya Mkono kwa Mkono unarudisha nyuma maendeleo ya vituo hivyo kwani mapolisi wanaohamishwa huwa tayari wameshapatiwa mafunzo, hivyo wanapoondoshwa inabidi Wizara ichukue juhudi mpya ya kuwapatia mafunzo mapolisi wengine wapya ambao watakapangiwa kutoa huduma katika vituo mbali mbali vya mkono kwa mkono (one stop centre).

5. Kamati imeweza kufahamu kuwa, tatizo la nauli kwa mashahidi linarudisha nyuma usikilizaji wa kesi katika mahakama za Mkoa. Pia kukosekana kwa ushahidi wa kitaalamu kunakwamisha mahakama hizo katika utoaji wa hukumu.

6. Pia Kamati imefahamu kuwa, uchache wa Mahakimu katika Mahakama za Mkoa kunachangia mrundikano mkubwa wa kesi katika mahkama hizo na tatizo la mashahidi kutowasili mahakamani kutoa ushahidi kunarudisha nyuma usikilizaji wa kesi.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kwa kuwa kumekuwa na ukosefu wa Kifaa cha DNA katika nchi yetu kwa kipindi kirefu, Kamati inaitaka Serikali kufanya ununuzi wa haraka wa kifaa hicho muhimu ili kisaidie katika kufanya uchunguzi wa kesi za udhalilishaji. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuwa, kesi za udhalilishaji ambazo ushahidi wake utakuwa unajitosheleza na hakuna ulazima wa kufanya uchunguzi wa kitaalamu zitolewe hukumu ili kupunguza mrundikano wa kesi za aina hiyo katika mahakama zetu.

2. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kuishajihisha jamii kuwa na muamko wa kufika mahakamani kwa ajili ya kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji ili ziwezwe kusikilizwa na kutolewa hukumu.

3. Kamati inaitaka Wizara, iwapo kutatokea uhamisho wa mapolisi katika vituo vya mkono kwa mkono, kuandaa utaratibu wa kuwaomba mapolisi waliokuwa washafanya kazi katika madawati ya jinsia ili kuondoa gharama ya kuanza kuwapatia mafunzo mapolisi wengine kwa vile mapolisi wanaotoka katika madawati ya jinsia wanakuwa na ujuzi wa kufanya kazi katika vituo hivyo.

**IDARA YA WANAWAKE NA WATOTO**

Kamati ilielezwa kuwa, Idara ya maendeleo ya Wanawake na Watoto ni Idara yenye jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Maendeleo ya wanawake na watoto Nchini. Aidha Idara inasimamia utekelezaji wa Haki za Wanawake na watoto na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mikataba ya Kimataifa inayohusu wanawake na watoto.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA WANAWAKE NA WATOTO**

1. Kamati imebaini ukosefu wa maafisa wa wanawake na watoto katika Wilaya unazorotesha utekelezaji na utoaji wa huduma zinazowahusu wanawake na watoto katika Wilaya.

2. Kamati imebaini kuwa kukosekana kwa usafiri wa Idara kunapelekea huduma zinazohitaji usafiri na ufuatiliaji kutofanyika kwa ufanisi. Hii inatokana na kuwa kuna maeneo mengine hususani katika Wilaya ya Kati yanakuwa ni magumu kufikika pindi kunapokosekana usafiri wa uhakika.

3. Kamati imetambua kuwa ufinyu wa ofisi unapelekea shughuli za ushauri nasaha na sheria kufanyika katika sehemu ambayo inakaliwa na watendaji wengine wa Idara ambapo kwa kawaida sehemu ya kutolea ushauri nasaha na huduma za sheria inatakiwa iwe yenye utulivu na usiri na isiwe na maingiliano na watu wengine.

4. Kamati imebaini kuwa, katika jitihada za idara za kuhamasisha wanawake kufanya shughuli za kiuchumi, idara imekuwa inapata muitikio mdogo wa wanawake hao katika kujiunga na vikundi vya kina mama hali inayorudisha nyuma jitihada za Idara. Aidha Kamati imebaini kuwa wanawake wengi bado hawajajitokeza katika kuchukua mikopo na wamekuwa na hofu katika kuchukua mikopo na kufanya biashara za kujiendeleza.

5. Kamati imebaini kuwa waratibu wa masuala ya wanawake na watoto wanafanya kazi kwa kujitolea bila ya kupata malipo yeyote lakini tatizo lililopo ni kuwa Idara inashindwa kuwadhibiti waratibu hao pindi wanapokuwa hawako tayari kuendelea na kazi za uratibu kwa kujitolea.

6. Pia Kamati imebaini kuwa, Idara inapata mashirikiano madogo na taasisi nyengine katika kufanya kazi zao.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

**1.** Kamati inaishauri Wizara kuomba nafasi za uajiri katika Ofisi ya Raisi, Kazi na Utumishi wa Umma za maafisa wanawake na watoto katika Wilaya ili kutatua tatizo la kukosekana kwa maafisa hao katika Wilaya zetu.

2. Kamati inaitaka Wizara kuandaa utaratibu wa kuwapatia motisha waratibu wa shughuli za wanawake na watoto ili idara iweze kuwadhibiti kwani wamekuwa wakifanya kazi na Idara ya Wanawake na Watoto kwa njia ya kujitolea na ni kiungo muhimu kati ya Wizara na shehia katika kufanikisha shughuli za Idara.

3. Kamati inaitaka Wizara kuipatia Idara sehemu maalum ya kutoa huduma ya ushauri nasaha na sheria ili wanawake na watoto wanaowasilisha malalamiko yao wapatiwe huduma katika sehemu hiyo maalum na ikiwa katika hali ya utulivu na usiri.

4. Licha ya kuwa Idara inapata muitikio mdogo wa wanawake katika kujishughulisha na shughuli za kiuchumi, Kamati inaitaka Idara kuendelea kuwahamasisha wanawake kufanya shughuli za kiuchumi ili kujiletea maendeleo.

**IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA**

Kamati ilielezwa kuwa, Idara ya Maendeleo ya Vijana ina jukumu la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana, kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar na kuhamasisha Vijana kujiunga katika kilimo cha kisasa cha uzalishaji wa mazao ya kilimo cha Rosela na Mboga mboga kwa Vijana wa Unguja na Pemba ili kujipatia ajira.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA**

1. Kamati imebaini kukosekana kwa Maafisa wa Wilaya kwa Unguja na Pemba kunazorotesha utekelezaji wa Sheria no 16 ya 2013 ya Uanzishwaji wa Baraza la Vijana kwani sheria hiyo imetaja wazi kuwa, katika utekelezaji wake kwa ngazi ya Wilaya, Maafisa Wilaya ndio watakuwa makatibu wa Mabaraza ya Wilaya.

2. Kamati imegundua ukosefu wa fedha za kutosha katika kutekeleza majukumu ya Idara hasa fedha za miradi ya maendeleo kumeipelekea Idara kushindwa kutatua changamoto zinazoikabili Idara katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano katika uendeshaji wa

Mradi wa Green House uliopo Tunguu kwa Unguja Idara imeshindwa kuwapatia Vijana wa Tunguu umeme wa jua katika kuendeleza utekelezaji wa shughuli zao za kilimo. Aidha kutokana na changamoto ya fedha Idara imekwamwa kutekeleza mradi wa aina hiyo uliyopo Pemba eneo la Mbuzini.

3. Kamati imebaini kuwa, Vijana bado hawako tayari kubadili mtazamo wao juu ya dhana ya Ajira kwani vijana walio wengi hawako tayari kujiajiri wenyewe au kushiriki katika sekta ya kilimo na hivyo wanategemea sana ajira Serikalini.

4. Kamati imebaini kuwa, kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika kunakwamisha shughuli za ufuatiliaji za Idara.

5. Kamati imebaini kuwa, Idara ina uhaba wa maafisa wa kutosha wenye sifa zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za idara.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Wizara kuomba nafasi za Uajiri za Maafisa Wilaya katika Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi kwasababu Sheria No. 16 ya mwaka 2013 ya uanzishaji wa Baraza la Vijana imetaja wazi kuwa Maafisa Wilaya ndio watakuwa makatibu wa Baraza la Wilaya. Hivyo kuzorotesha ajira zao kutakwamisha utekelezaji wa sheria hiyo.

2. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara, fedha zake za bajeti kama zilivyoidhinishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa fedha za miradi kwani uingiaji mbaya wa fedha unazorotesha utekezaji wa kazi za kawaida za Wizara na kazi za maendeleo. Hali hii imejidhihirisha katika utekezaji wa mradi wa Gree House ambao utekelezaji wake haujafikia malengo yaliyokusudiwa.

3. Kamati inaitaka Wizara kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Idara ya Vijana ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha Kamati inaitaka Idara kuendelea kuwashajihisha vijana kushiriki katika sekta ya kilimo kwasababu ina tija na itapunguza idadi ya vijana wanaodhurura mitaani bila ya ajira.

**IDARA YA USTAWI WA JAMII**

Kamati ilielezwa kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii inaendelea kufanya kazi ya kuhakikisha kuwa huduma za kiustawi zinatolewa kwa watoto na wazee wanaoishi katika mazingira magumu. Aidha Kamati ilielezwa kuwa, Idara katika utekelezaji wa shughuli zake bado inakabiliwa na changamoto.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA USTAWI WA JAMII**

1. Kamati imebaini kuwa Idara haipatiwi pesa za posho kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wanaozika maiti zisizokuwa na wenyewe. Kamati imebaini kuwa wafanyakazi wanaozika maiti zisizokuwa na wenyewe wanafanya kazi hiyo katika mazingira magumu na wanahitaji kupatiwa posho ili kuwatia moyo. Aidha Kamati imebaini kuwa, maiti zimekuwa hazina sehemu nzuri ya kuhifadhiwa kutokana na kuwa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali kuu ya Mnazi mmoja ni kibovu na kichakavu hali inayopelekea uhifadhi mbaya wa maiti hizo.

## MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

**1.** Kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara ya Afya fedha za kukifanyia matengenezo makubwa chumba cha kuhifadhia maiti kilichopo Hospitali kuu ya Mnazi mmoja kutokana na kuwa, chumba hicho ni kibovu, kimechakaa na hakiridhishi. Kufanya hivyo kutapelekea maiti kuhifadhiwa vizuri maiti katika chumba hicho.

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kamati ilifanya ziara katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kupokea taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai/Septemba 2014/2015 kwa upande wa Pemba na kwa Unguja ilifanya kazi kwa kipindi cha Oktoba/Disemba 2014/2015. Kamati katika kazi zake miongoni mwa maeneo waliloyatembelea ni Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (Skuli ya Tiba na Sayansi ya Afya), Taasisi ya Karume na Sayansi na Teknolojia, Skuli ya Dimani, Skuli ya Mfuru Matonga, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu, Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo na Kituo cha Elimu ya watu wazima Forodhani.

Kamati katika ziara zake iligundua changamoto mbali mbali ambazo inaikabili Wizara hii kupitia maeneo ambayo Wizara inazisimamia. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Kamati imebaini kukosekana kwa hatimiliki kwa maeneo ya Wizara na Taasisi za Serikali kukosa kupewa kipaombele katika kupatiwa hatimiliki ni moja ya sababu zinazopelekea maeneo ya Wizara kuendelea kuchukuliwa kama vile ilivyo katika eneo la chuo cha Kiislam Mazizini hali inayochangia kuibuka kwa migogoro ya ardhi katika jamii.

2. Kamati imegundua kuwa Wizara inakabiliwa na changamoto ya fedha kwa taasisi inazosimamia kama vile Taasisi ya Karume na Sayansi na Teknolojia, Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo, Kituo cha Elimu ya Watu Wazima Forodhani, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar hali inayokwamisha utekelezaji wa majukumu ambayo yamepangwa katika taasisi au vituo hivyo.

3. Kamati ilipotembelea Skuli ya Dimani ilibaini kuwa miundombinu ya mafeni iliyoingizwa katika madarasa ya Skuli hiyo yanahatarisha usalama wa wanafunzi kwasababu dari ya skuli ipo chini sana ukilinganisha na kiwango kinachohitajika hivyo kupelekea mafeni kuwa karibu na madawati ambayo wanafunzi wanakaa.

4. Kamati imebaini kuwa mradi wa lishe maskulini bado unakabiliwa na changamoto ya muitikio mdogo wa wazazi katika kufanikisha mradi huo. Hali hiyo imejitokeza katika Skuli ya Mfuru Matonga ambapo baadhi ya wazazi wamekuwa wakitoa mashirikiano madogo katika kufanikiasha mradi huo hasa katika suala la uchangiaji wa fedha za kuwalipa wapishi.

5. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutopatiwa fedha ipasavyo zinazotokana na kodi ya Bandari kwa vipindi vya miaka miwili mfulilizo tokea kodi hiyo kuanza kukusanywa na Wizara ya Fedha. Kamati ilibaini kuwa katika mwaka wa fedha **2012/2013**, Wizara ilipangiwa kupatiwa bilioni mbili **(2,000,000,000)** baada ya makusanyo lakini fedha waliopatiwa Wizara ni shilingi milioni mia tatu na arubaini tisa, laki moja na elfu thamanini **(349,180,000).** Aidha katika mwaka wa fedha wa **2013/2014** Wizara ilitengewa bilioni mbili

**(2,000,000,000**) na fedha waliyopatiwa ni shilingi milioni mia saba na hamsini na sita, laki tatu arubaini na mbili elfu, mia nane na thalathini (**756,342,830**). Katika mwaka wa fedha wa **2014/2015** Wizara ilipangiwa kupatiwa bilioni mbili **(2,000,000,000)** lakini mpaka kufikia kota ya pili fedha zilizopatikana ni shilingi Milioni mia tatu hamsini na moja, laki tatu na hamsini na moja elfu **(351,351,000)**. Kutokana na uingizwaji mbaya wa fedha za kodi ya bandari, ni dhahiri kuwa Wizara itashindwa kufikia malengo yake ya kutatua tatizo la vikalio (madawati) maskulini.

6. Kamati imefurahishwa na jitihada za Wizara kwa kuandaa mtaala mpya wa masomo kwa shule za msingi ambao ulianza kutumika tangu mwaka 2010 kwa lengo la kufuta darasa la saba na kupelekea elimu ya msingi kuishia darasa la sita. Hatahivyo Kamati imesikitishwa baada ya kubaini kuwa licha ya mtaala kuanza kutumika tokea mwaka 2010, Wizara haikufanya maandalizi ya kutosha katika kuwaandaa walimu kimafunzo ikiwa ni pamoja na kuwapatia vifaa vya kufundishia (vitabu). Aidha kwa upande wa wanafunzi ambao wanatarajiwa kufanya mtihani wa darasa la sita katika mwaka huu wa 2015, inaonekana bado hawana uwezo wa kukabiliana na mtihani huo kutokana na kukosa maandalizi ya kutosha.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Serikali kuzipa kipaumbele taasisi zake katika kuzipatia hatimiliki ili kuepusha uvamizi wa maeneo yake pamoja na kuepusha migogoro inayojitokeza katika jamii.
2. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua ya kuzikagua upya shule mpya zilizojengwa ikiwemo Skuli ya Dimani ili kurekebisha kasoro mbali inazojitokeza katika majengo ya skuli hizo na kuzinusuru.
3. Kamati inaitaka jamii kuunga mkono jitihada za Serikali na wafadhili za kuazisha mradi wa lishe maskulini kwa Unguja na Pemba ili mradi huo uendelee na wanafunzi wanufaike. Kamati imepata matumaini makubwa kuwa kuendelea kwa mradi huo kutapelekea wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao na kupunguza tatizo la utoro maskulini kama ilivyobainika kwa baadhi ya skuli ambazo mradi huo unaendelea.
4. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kuipatia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali fedha za kodi ya Bandari kwa ukamilifu wake ili Wizara iweze kutengenezesha madawati na kuondoa changamoto ya uhaba wa madawati maskulini. Aidha Kamati inataka Wizara ya Fedha kuipatia Wizara ya Elimu na Mafunzo Amali mchanganuo halisi wa fedha za kodi ya madawati wanayokusanya ili Wizara ipange mipango yake ya matumizi kwa mujibu wa fedha zinazopatikana.
5. Kamati inaiagiza Wizara kuwapatia walimu wa shule za msingi mafunzo ya kutosha kuhusiana na mtaala mpya na kuharakisha ukamilishaji wa vitabu vya kufundishia ili walimu wa shule zote za msingi watumie vitabu vya aina moja kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi kupata vitabu vya kujisomea.

**KITUO CHA ELIMU MBADALA RAHALEO**

Kamati ilitembelea kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo na kuelezwa kuwa kituo hicho kimeanzishwa kutokana na kuimarika kwa madarasa ya Elimu Mbadala yaliyoanzishwa katika baadhi ya Skuli za Serikali za Unguja na Pemba. Aidha Kamati ilielezwa kuwa

malengo ya kituo hicho ni kuwapatia elimu vijana bila ya ubaguzi wa aina yeyote na kutoa elimu yenye manufaa kwa wanafunzi ili kuwenda sambamba na mpango mzima wa kupunguza umaskini nchini.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KITUO CHA ELIMU MBADALA RAHALEO.**

1. Kamati imebaini ukosefu wa walimu wa kudumu wa fani mbali mbali katika kituo unapelekea wanafunzi kutokuwa na uhakika wa kusomeshwa masomo yao pindi wanapokuwa kituoni hapo.
2. Kamati ilipokuwa inafanya ziara katika kituo, iliweza kufahamu kuwa kituo hakina "workshop' kwa ajili ya kufanyia mazoezi ya vitendo kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya fani kama vile fani ya uchongaji na fani ya ushoni.
3. Kamati iliweza kufahamu kuwa Kituo hakina vifaa vya kutosha kwa ajili ya kufundishia.
4. Kamati imebaini kuwa kituo kina uhaba wa fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya chuo.
5. Kamati imebaini kuwa, wanafunzi wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Rahaleo wanakosa fursa ya kujiunga na kujiendeleza katika Kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni pindi wanapokamilisha masomo yao. Hali hii imetokana na mabadiliko ya sifa na vigezo vinavyotumika katika kupatiwa nafasi ya kujiunga katika kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni.

**KITUO CHA ELIMU YA WATU WAZIMA FORODHANI**

Kamati ilitembelea kituo cha Elimu ya watu wazima Forodhani na imebaini kuwa jamii imeshajihika katika kujiunga na kituo hasa wanawake. Kamati ilielezwa kuwa kituo kimepata mafanikio ya kusomesha wanafunzi katika kada ya ushoni, mapishi, uchongaji na fani nyengine ambapo baadhi ya wanafunzi wanapomaliza masomo yao hupata fursa wa kuajiriwa na wengine hujiari wenyewe. Kwa upande wa changamoto Kamati ilielezwa kuwa kituo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Kamati imebaini kuwa kituo kinakabiliwa na ukosefu wa fedha ambapo kwa kipindi cha Julai/Disemba fedha zilizopatikana zimefikia asilimia 32.6% ya fedha zilizotarajiwa kuingizwa.
2. Kamati imegundua upungufu wa walimu katika fani ya uchongaji na sayansikimu.
3. Pia Kamati imejionea uchakavu wa jengo la kituo ambalo kutokana na hali yake, linahitaji kufanyiwa ukarabati kwani jengo ni la zamani. Pia Kamati imebaini kuwa sehemu inayotumika kufundishia fani ya uchongaji ukuta wake ni mbovu na usipofanyiwa matengenezo ya haraka unaweza kuleta athari kwa wanafunzi na jamii iliyozunguka eneo hilo.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Wizara kupanga mikakati ya kukipatia kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo na Kituo cha Elimu ya Watu wazima Forodhani walimu wa kutosha kwa fani mbali mbali hasa fani ya uchongaji kwani fani hiyo ina upungufu mkubwa wa walimu. Kamati imebaini kuwa

vituo vyote vina ukosefu wa mwalimu wa fani ya uchongaji ambapo katika kituo cha Rahaleo yupo mwalimu mmoja ambaye anakaribia kustaafu na kwa upande wa kituo cha Elimu ya watuwazima cha Forodhani hakuna hata mwalimu mmoja.

2. Kamati inaitaka Wizara kupitia upya dhamira za kuanzishwa kwa Kituo cha Elimu Mbadala cha Rahaleo na Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni ili kuweza kubaini mahusiano yaliyopo baina ya vituo hivyo viwili na kutatua mapungufu yanayojitokeza ambayo yanapelekea kuwanyima fursa wanafunzi waliomaliza mafunzo yao katika Kituo cha Elimu Mbadala cha Rahaleo kuweza kujiendeleza katika Kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni wakati dhamira ya mwanzo ni kuwa wanafunzi wanapomaliza kituo cha Rahaleo wapate fursa ya kuendelea na masomo yao katika kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni.

3. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa kituo cha Rahaleo kinapatiwa eneo la workshop ili wanafunzi wa fani wapate mazoezi ya vitendo na hatimae kujenga ufahamu mzuri wa fani zao.

4. Kamati inaitaka Wizara kuchukua hatua za haraka za kufanya matengenezo ya ukuta katika kituo cha Elimu ya Watu Wazima Forodhani. Aidha Kamati inaishauri Wizara kuandaa mpango wa muda mrefu wa kukifanyia ukarabati kituo kwani majengo yake ni ya zamani yanahitaji kukarabatiwa.

**BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR**

Kamati ilipotembelea Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, ilielezwa kuwa Bodi imeanzishwa kwa Sheria namba 3 ya 2011 kufuatia kufutwa kwa Sheria Namba 6 ya 2001 ya Mfuko wa Elimu ya juu na kurithi kazi za mfuko huo. Malengo ya Mfuko ni utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa wanafunzi wanajiunga na Vyuo vya Elimu ya juu.

**CHANGAMOTO INAZOZIKABILI BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR**

**1. Upungu wa Fedha za kuwakopesha wanafunzi ukilinganisha na wingi wa maombi ya mikopo kwa kila mwaka**

Kamati ilielezwa kuwa, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita wastani wa wanafunzi wanaoteuliwa kukopeshwa ni kati ya 26% mpaka 32% wakati zaidi ya 68% ya waombaji hawapati mikopo na wengine kushindwa kuendelea na masomo pamoja na kuwa wamekubaliwa kujiunga na vyuo vikuu.

**2. Kukosekana kwa fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi na kusababisha Bodi kuhamisha madeni katika bajeti mpya zinazofuata**

Kamati imeelezwa kuwa, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo fedha zinazoingizwa kutoka mfuko mkuu wa Serikali ni kati ya 57% mpaka 67% na kuisababisha Bodi kurithi madeni ya miaka ya nyuma na hivyo kudhoofisha uwezo wa bajeti mpya ya Bodi na kupunguza idadi ya uteuzi wa vijana wapya.

3. **Fedha kuchelewa na kupatikana nje ya wakati**

Kamati imeelezwa kuwa, ucheleweshwaji wa fedha hupelekea malalamiko na usumbufu mkubwa kwa wanafunzi. Kamati ilipokea maelezo kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa miezi minane Bodi ilikadiriwa kupatiwa shs 9.3 bilioni na kilichopatikana ni shs 3.4 bilioni na uwezekano wa kupata fedha iliyobakia shs 5.9 bilioni kwa miezi mine iliyobakia ni mdogo sana.

4. **Urejeshaji mikopo kwa wanafunzi waliokopeshwa kuanzia mwaka 2006 – 2014 hauridhishi ukilinganisha na fedha zilizotolewa na Serikali ambazo zimefikia Tshs 25 bilioni kwa miaka 13 iliyopita.**

   Kamati imeelezwa kuwa kiwango cha makusanyo (marejesho) hakiridhishi kutokana na kuwa Bodi inapata mashirikiano madogo kwa baadhi ya taasisi, baadhi ya wakopaji wanakana madeni yao, Bodi inapata ugumu wa kufahamu wakopaji waliopata ajira za taasisi binafsi, kuhama kwa baadhi ya wadaiwa kwenda nje na Tanzania bara na kutokufahamu umuhimu wa kulipa madeni kwa baadhi ya wakopaji kunazorotesha kiwango cha makusanyo.

5. **Ufinyu wa Nafasi** Kamati ilipotembela Bodi ilibaini kuwa jengo wanalotumia ni finyu ukilinganisha na shughuli zinazotekelezwa. Kamati imebaini hali nhiyo katika sehemu ya kuhifadhia mafaili, sehemu ya wageni na ukumbi wa mikutano.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kwa kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar inakabiliwa na upungufu wa fedha za kuwakopesha wanafunzi, Kamati inashauri Taasisi nyengine za fedha za Zanzibar zianzishe utaratibu wa kutoa mikopo ya Elimu ya juu kwa makundi ya jamii ili kupunguza vijana wengi kutegemea Bodi ya Mikopo pekee. Miongoni mwa taasisi ambazo Kamati inapendekeza ni Benki ya Watu wa Zanzibar ya Kiisalamu ianzishe mashirikiano na vyuo vya ndani kwa kumkopesha mwanafunzi au mzee wa mwanafunzi ada na gharama za kujikimu. Aidha Kamati inapendekeza Mfuko wa Hifadhi wa Jamii wa Zanzibar uanzishe utaratibu wa kuwakopesha gharama za masomo wanafunzi wanaohitaji kujiendeleza masomo yao ambao hawana uwezo wa kujilipia na ambao ni wanachama wa mfuko au wazee wa wanafunzi hao ni wanachama wa mfuko huo.

2. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Bodi, fedha kama zilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi ili kuepusha Bodi kurithi madeni ya miaka ya nyuma katika bajeti mpya hali itakayopelekea kuzorotesha utekelezaji wa majukumu ya Bodi.

3. Kamati imebaini ucheleweshaji na upatikanaji wa fedha za Bodi nje ya wakati hali inayowapa wakati mgumu wanafunzi wanaotegemea mkopo huo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha kodi ya kuchangia elimu ya juu na fedha zitakazopatikana zisaidie Bodi kuwapatia wanafunzi mikopo kwa wakati kama sheria zitakavyoelekeza.

4. Kamati inaitaka Wizara kuweka mkakati wa kuipatia Bodi ya Elimu ya Juu Zanzibar jengo la kutosha ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

**OFISI KUU PEMBA**

Kamati ilikutana na Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali – Pemba na kupokea taarifa ya utekelezaji pamoja na kutembelea Ofisi ya Takwimu, Kituo cha Elimu Mbadala Wingwi, Skuli ya Kojani, Skuli ya Chambani na Skuli ya Furaha. Kamati ilibaini changamoto mbali mbali katika maeneo waliyoyatembelea kama hivi zifuatavyo:-

1. Kamati imebaini uingizwaji mbaya wa fedha katika Wizara na fedha wanazoingiziwa hazifikii hata asilimia hamsini za fedha zote za bajeti walizopangiwa.
2. Kamati imesikitishwa na malimbikizo ya posho za walimu 145 na kukatwa kwa fedha za mshahara za walimu 159 ambazo malipo yake tayari yameizinishwa na Ofisi ya Raisi, Kazi na Utumishi wa Umma kwa barua ya tarehe 10/09/2012 lakini utekelezaji wake umekwama Wizara ya fedha Unguja.
3. Kamati inasikitishwa sana na Ofisi za Wakaguzi Pemba kwani hairidhishi na watendaji wa Ofisi hiyo wanafanya kazi katika mazingira magumu.
4. Kamati imebaini kuwa, Ofisi kuu Pemba ina madeni makubwa ya umeme na maji katika Taasisi zake na watendaji wa Ofisi wameieleza Kamati kuwa, madeni hayo ni makubwa sana na wana wasi wasi nayo kwani ni kinyume na matumizi yao halisi.
5. Kamati imebaini kuwa baadhi ya skuli zinakabiliwa na kesi za ujauzito na ndoa kwa wanafunzi.
6. Kamati imebaini kuwa malipo ya fidia za vipando katika eneo la Vitongoji ambalo lilijengwa chuo cha Amali bado hayajakamilika.

**OFISI YA TAKWIMU**

1. Kamati imebaini kuwa, kukosekana kwa air condition (kiyoyozi) katika ofisi ya takwimu kunahatarisha usalama wa computa zilizopo ambazo zinahitaji ubaridi, taarifa zenyewe zinazohifadhiwa na hata afya za wafanyakazi kwani hewa inakuwa haizunguki vizuri kutokana na ufinyu wa chuma hicho.
2.

**SKULI YA KOJANI**

1. Kamati ilipotembelea skuli ya Kojani imesikitishwa sana hali ya kukosekana kwa walimu wa sayansi kwa kipindi kirefu tokea mwaka 2009 hadi sasa na kupelekea wanafunzi kutosomeshwa masomo ya sayansi na kuwanyima fursa wanafunzi wanaopenda masomo yao.
2. Pia Kamati imebaini uhaba wa madarasa katika skuli ya kojani kwani jamii hiyo imekuwa na muamko mkubwa wa kuwapeleka watoto maskulini lakini madarasa yaliyopo hayatoshelezi.

**SKULI YA CHAMBANI MSINGI**

1. Kamati ilipotembelea Skuli ya Chambani imebaini uhaba wa walimu na kupelekea idadi ya madarasa kuwa haiwiani na walimu waliopo na hivyo walimu kushindwa kumudu kufundisha madarasa yote kwa ufanisi. Kamati ilibainishiwa kuwa, skuli ina walimu 19 na idadi ya madarasa ni 21.
2. Kamati imesikitishwa sana baada ya kubaini kuwa, wanafunzi wa skuli ya maandalizi ya Chambani hawana madarasa hali inayopelekea wanafunzi hao kusoma maeneo tofauti na hata vifaa vyao vya kufundishiwa kukosa sehemu maalumu ya kuhifadhiwa.

3. Kamati imebaini kuwa, skuli haina hatimiliki hali inayoweza kusababisha kuzuka kwa migogoro ya ardhi katika maeneo ya skuli.
4. Pia Kamati imebaini kuwa, skuli haina walinzi hali inayoweza kusababisha wizi wa vifaa na uvamizi wa maeneo ya skuli.

**SKULI YA FURAHA**

1. Kamati ilipofanya ziara katika Skuli ya Furaha imebaini uchakavu wa majengo ya skuli, ukosefu wa vifaa vya maabara na kukosekana kwa walinzi katika maeneo ya skuli.
2. Pia Kamati imebaini uhaba wa walimu hasa mwalimu wa somo la biology.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Wizara kuisaidia Ofisi kuu Pemba katika kufuatilia fedha za malimbikizo ya posho za likizo za walimu 145 zenye thamani ya Tshs 136,231,000/= na fedha zilizokatwa za mshahara za walimu 159 zenye thamani ya Tshs 18,487,900/= ambazo zimekwama Wizara ya Fedha Unguja na idhini ya malipo imeshatolewa na Ofisi ya Raisi, Kazi na Utumishi wa Umma kwa barua ya tarehe 10/09/2012.
2. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara, fedha za bajeti Kama zilivyoidhinishwa ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
3. Kamati inaitaka Wizara kuboresha Ofisi za Wakaguzi Pemba ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.
4. Kamati inaitaka Wizara ya Elimu Pemba kufanya mazungumzo na Shirika la Umeme lililopo Pemba ili waweze kufahamu madeni yao ya umeme na maji na kuweza kuondoa utata uliopo katika madeni hayo.
5. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kuelimisha jamii katika kuwapa malezi bora watoto wao ili kuwaepusha na ndoa za mapema na kujihusisha katika vitendo vitakavyopelekea kupata ujauzito wakiwa shuleni.
6. Kamati inaishauri Wizara kuwa makini katika ulipaji wa deni la fidia la vipando kwa wananchi wa Vitongoji ili kuepusha kuzuka kwa migogoro katika jamii na kujitokeza watu wasiohusika kutaka kupewa malipo ya fidia.
7. Kamati inaitaka Wizara kuifanyia marekebisho Ofisi ya Takwimu kwa kuweka air condition ambazo zitasaidia katika kuzitunza computa zilizopo, uhifadhi wa takwimu zenyewe na kulinda afya za watendaji wa kitengo hicho.
8. Kamati inaitaka Wizara kuipa kipaumbele skuli ya kojani kwa kuipatia walimu wa sayansi kwani kwa kipindi kirefu wanafunzi wa skuli hiyo wamekosa kusoma masomo ya sayansi na inawanyima fursa wanafunzi wanaopenda masomo hayo.
9. Kamati inaitaka Wizara kuipatia Skuli ya Chambani jengo maalum la kufundishia wanafunzi wa maandalizi kwani kwasasa hawana jengo na wamekuwa hawana utulivu wa masomo yao kutokana na kuhama hama.

## SEHEMU YA TATU

## HITIMISHO

Kwa ujumla, hali ya mapato ya Serikali inaonekana kuongezeka mwaka hadi mwaka kwa mujibu wa takwimu zinazoonyesha mapato yote yanayokusanywa na Serikali.Hatahivyo, ongezeko hilo la mapato halionekani kuleta unafuu katika upande wa matumizi kwani wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii bado zimeendelea kuathirika na tatizo sugu la kutoigiziwa fedha kwa wakati kwenye kasma za vifungu vyao vilivyopitishwa katika bajeti**.** Nidhamu katika matumizi ya fedha za Umma ni miongoni mwa nguzo muhimu katika uendeshaji wa shughuli za Serikali ya kidimokrasia. Hivyo Kamati inashauri fedha zipelekwe sehemu husika na kwa wakati ili Wizara ziweze kutekeleza majukumu waliyojipangia.

Kamati katika kusimamia utekelezaji wa wizara hizi, imebaini juhudi za Wizara zote katika utekelezaji wa majukumu yake, licha ya kukabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Kamati imebaini kuwa, Wizara ambazo inazimamia zinapatiwa bajeti ndogo na ambayo haingizwi kama ilivyopitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na hivyo utekelezaji wa malengo waliyojipangia kwa asilimia kubwa ni kupitia michango ya washirika wa maendeleo. Iwapo Serikali imelenga kuimarisha afya nchini, kukuza Ustawi wa Jamii na kuwaendeleza wanachi wake kielimu ni lazima wizara hizi zipatiwe fedha zake za bajeti ipasavyo.

Kamati inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa watendaji wote wa Idara na Taasisi ambali kwa mashirikiano waliyoipatia wakati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake na kufanikisha kuandaa ripoti hii. Aidha Kamati inatoa shukrani kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu na Watendaji wote wa Baraza laWawakilishi kwa kwa kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.